ISSN 0856-6976

TAMKO LA SERA YA FEDHA

Mapitio ya Nusu Mwaka

2025/26

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Februari 2026

ISSN 0856-6976

TAMKO LA SERA YA FEDHA

Mapitio ya Nusu Mwaka

2025/26

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Februari 2026

5 Februari 2026

Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb),
Waziri wa Fedha,
Mji wa Serikali-Mtumba,
Barabara ya Hazina,
S. L.P 2802,
40468 Dodoma.

Mheshimiwa Waziri,

BARUA YA WASILISHO

Kifungu namba 21, cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, kinaitaka Benki Kuu ya Tanzania kutoa **Tamko la Sera ya Fedha** mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka ambayo hutolewa mwezi Februari. Tamko hili huainisha mwelekeo wa sera ya fedha na utekelezaji wake katika kufikia malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali. Kwa muktadha huo, nawasilisha kwako **Mapitio ya Nusu Mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2025/26**, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Tamko hili la Sera ya Fedha linatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Vilevile, Tamko hili linabainisha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na mwelekeo wa sera ya fedha kwa nusu ya pili ya mwaka 2025/26, katika kufikia malengo yake.

Wasalaam,

Emmanuel M. Tutuba
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

YALIYOMO

BARUA YA WASILISHO .... **i**
MUHTASARI iv

SEHEMU YA KWANZA **1**
1.0 UTANGULIZI 1

SEHEMU YA PILI **4**
2.0 MSIMAMO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA 4
2.1 Msimamo wa sera ya fedha 4
2.2 Utekelezaji wa sera ya fedha 5

SEHEMU YA TATU **7**
3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA 7
3.1 Mwenendo wa shughuli za uzalishaji 7
3.2 Mfumuko wa bei 8
3.3 Mwenendo wa bei za bidhaa 10
3.4 Mwenendo wa Masoko ya Fedha Duniani 14

SEHEMU YA NNE **15**
4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI 15
4.1 Pato la Taifa 15
4.2 Mfumuko wa Bei 18
4.3 Viwango vya Riba 22
4.4 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi 23
4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali 26
4.6 Deni la Serikali 29

4.7 Mwenendo wa Urari wa Malipo ya Kawaida 32
4.8 Mwenendo wa Ukwasi wa Fedha za Kigeni, Thamani ya Shilingi na Akiba ya Fedha za Kigeni 40
4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha 43
4.10 Mifumo ya Malipo 44

SEHEMU YA TANO 47
5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI 47
5.1 Mwelekeo ya Uchumi wa Dunia 47
5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani 49

SEHEMU YA SITA 51
6.0 SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA PILI YA MWAKA 2025/26 51

VIAMBATISHO 53
TAFSIRI YA DHANA MUHIMU 59

MUHTASARI

Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26

Katika kutimiza jukumu la kuandaa na kutekeleza sera ya fedha, Benki Kuu ilitoa Tamko la Sera ya Fedha mwezi Juni mwaka 2025, ambalo linabainisha kuwa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26 inalenga kuongeza ukwasi ili kuwezesha ukuaji wa uchumi. Mwelekeo huo wa sera ya fedha ulitokana na mfumuko wa bei kutarajiwa kuwa ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Kwa kuzingatia mwelekeo huo, mwezi Julai 2025, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Benki Kuu ilipunguza Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 6 hadi asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2025. Kutokana na mfumuko wa bei kutarajiwa kuendelea kuwa ndani ya lengo, kikao cha Kamati ya Sera ya Fedha kilichofanyika mwezi Oktoba 2025 kiliamua kuendelea na riba ya asilimia 5.75 katika robo ya mwaka inayoishia Desemba 2025.

Kwa kuzingatia maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha, Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha kwa kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki za biashara (*7-day interbank rate*), ambayo ni kiashiria cha ukwasi unaohitajika kwa shughuli za uchumi, inakuwa ndani ya wigo wa asilimia ± 2 ya Riba ya Benki Kuu. Katika kufikia lengo hili, Benki Kuu ilitumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha kwa ufanisi na kufanikiwa kupata matokeo yaliyokusudiwa, ambapo ukwasi katika benki za biashara uliongezeka na riba ya mikopo ya siku saba ilipungua na kuwa ndani ya wigo wa asilimia ± 2 ya Riba ya Benki Kuu. Mafanikio haya yanaashiria kuongezeka kwa ufanisi wa sera ya fedha katika kufikia malengo ya kuwa na mfumuko wa bei mdogo na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mwenendo wa uchumi wa dunia

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa mwanzoni mwa Januari 2026, uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 ulikuwa imara, licha ya kuwepo kwa changamoto zilizotokana na migogoro ya kisiasa, kuongezeka kwa ushuru wa forodha kwa baadhi ya nchi, na kutotabirika kwa sera za kiuchumi. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.3 katika mwaka 2025, kama ilivyokuwa mwaka 2024. Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, ambapo baadhi ya nchi ziliweza au kukaribia kufikia malengo yaliyowekwa na benki kuu husika. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa sera za fedha iliyolenga kupunguza ukwasi katika kipindi kilichopita, pamoja na kupungua kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia. Mwenendo wa bei za bidhaa katika soko la dunia ulikuwa wa mwelekeo tofauti. Mathalani, bei ya dhahabu iliongezeka kwa kasi na kufikia kiwango cha juu zaidi kuwahi kufikiwa cha zaidi ya dola za Marekani 4,309 kwa wakia mwezi Desemba 2025. Kwa upande mwingine, bei ya mafuta ghafi ilishuka hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 64.8 kwa pipa. Ongezeko la bei ya dhahabu linatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dhahabu kwa kuwa inachukuliwa kama akiba iliyo salama zaidi wakati wa misukosuko ya kiuchumi. Bei ya mafuta ghafi ilipungua kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji huku mahitaji yakipungua.

Mwenendo wa uchumi wa Tanzania

Uchumi umeendelea kuwa imara na stahimilivu, ikichangiwa na wigo mpana wa mjengeko wa shughuli za uchumi. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2025, na unakadiriwa kukua kwa takriban asilimia 5.9 kwa mwaka mzima kutokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za uchumi kwa robo ya nne. Kasi hiyo ya ukuaji wa uchumi ni zaidi ya ukuaji wa asilimia 5.5 katika mwaka 2024 na ulikuwa karibu

sawa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6. Ukuaji huo ulichangiwa na sekta mbalimbali za uchumi, hususan kilimo, ujenzi, na madini. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 6.7 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2025, ukichangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi, na uzalishaji viwandani, na unakadiriwa kukua kwa asilimia 6.8 kwa mwaka mzima kutokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za uchumi katika robo ya nne.

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa mdogo na tulivu katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Kwa upande wa Tanzania Bara, mfumuko wa bei ulikuwa kati ya asilimia 3.1 hadi asilimia 3.6, ikiwa ndani ya lengo la wigo wa asilimia 3 hadi 5. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 3.7. Mwenendo huo wa mfumuko wa bei mdogo ulitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, utulivu wa bei hususan bei za chakula, pamoja na kuimarika kwa thamani ya shilingi. Aidha, hali hii ilitokana na kupungua kwa bei za bidhaa za walaji zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, ikiwemo bei za mafuta katika soko la dunia.

Viwango vya riba katika benki za biashara viliendelea kuwa tulivu, ambapo riba za mikopo zilikuwa wastani wa asilimia 15, na riba za mikopo kwa wateja wakubwa na wale wanaoaminika zaidi zilikuwa takribani asilimia 13. Riba za amana zilikuwa wastani wa asilimia 9. Ujazi wa fedha uliendelea kukua hadi kufikia asilimia 21.8, kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi, pamoja na kuimarika kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Aidha, mikopo inayotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 17.6. Hali hii inaashiria kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi na biashara.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika nusu ya kwanza ya 2025/26 ulikuwa wa kuridhisha. Mapato ya ndani kwa upande wa Tanzania Bara

yaliongezeka na kuwa zaidi ya lengo kwa takriban asilimia 3.8. Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya Serikali yalivuka lengo kwa asilimia 1.9. Mafanikio hayo yanaashiria kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, sanjari na kukua kwa shughuli za kiuchumi. Matumizi kwa Serikali zote mbili yaliendelea kufanyika kwa kuzingatia upatikanaji wa mapato. Deni la Serikali liliendelea kuwa himilivu, huku kiwango cha kiashiria cha uhatarishi kikibaki kuwa cha wastani. Kutokana na takwimu za mwaka 2024/25, uwiano wa thamani ya sasa ya deni kwa Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 40.7 kutoka asilimia 41.1 katika mwaka uliotangulia. Kiwango hiki ni chini ya ukomo wa uhimilivu wa deni wa asilimia 55.

Sekta ya nje iliendelea kuimarika na kuwa himilivu zaidi, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inakadiriwa kupungua hadi kufikia asilimia 2.2 ya Pato la Taifa, ikiwa ni kiwango cha chini zaidi kufikiwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Mwenendo huo ulichangiwa zaidi na ongezeko kubwa la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususani dhahabu, utalii, shughuli za usafirishaji, mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani. Aidha, kupungua kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia kulichangia kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuwa na ziada kutokana na shughuli za utalii na kupungua kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Ukwasi wa fedha za kigeni ulikuwa wa kutosha kutokana na ongezeko la fedha za kigeni kutoka vyanzo mbalimbali, hususan mauzo ya dhahabu, utalii, mazao ya kilimo na usafirishaji. Shilingi iliendelea kuimarika dhidi ya fedha za kigeni, ambapo iliongezeka thamani kwa asilimia 5.5 dhidi ya dola ya Marekani. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.3, ambapo takriban asilimia 13 ilikuwa dhahabu fedha. Akiba hiyo ilikuwa inatosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 4.9, ikiwa ni zaidi ya lengo la miezi 4 au zaidi.

Sekta ya fedha iliendelea kuwa imara, thabiti na yenye uwezo wa kuhimili mitikisiko ya muda wa kati na mfupi, huku viashiria vyote vikiwa ndani ya wigo unaokubalika. Sekta ya benki, ilikuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha, na yenye kutengeneza faida. Ubora wa rasilimali za benki za biashara uliendelea kuimarika, kufuatia kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) dhidi ya mikopo yote hadi asilimia 2.8 mwezi Desemba 2025, chini ya kiwango kinachohimilika cha asilimia 5. Mifumo ya malipo ilikuwa imara, ikiendelea kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuwezesha shughuli za kiuchumi. Benki Kuu iliendelea kuboresha mifumo ya malipo pamoja na kutekeleza hatua za kuongeza matumizi na upatikanaji wa mifumo. Aidha, Benki Kuu iliendelea kusimamia utekelezaji wa miongozo na maelekezo mbalimbali kuhusu upangaji wa tozo na gharama za huduma za malipo ya kidigitali, ili kuhakikisha huduma hizo zinakuwa nafuu kwa watumiaji.

Matarajio ya uchumi kwa nusu ya pili ya mwaka 2025/26

Uchumi wa dunia

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kuwa himilivu licha ya kuwepo kwa changamoto za migogoro ya kisiasa, kuongezeka kwa ushuru wa forodha na hali ya kutotabirika kwa sera za kiuchumi duniani. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linatarajia uchumi wa dunia kuendelea kukua kwa kasi ya asilimia 3.3 mwaka 2026, juu kidogo kwa asilimia 0.2 ikilinganishwa na makadirio ya awali yaliyofanyika mwezi Oktoba 2025. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na kupungua kwa bei za nishati, na kupungua kwa changamoto za usafirishaji. Kutokana na mwenendo huo, benki kuu zinatarajiwa kuendelea kupunguza viwango vya riba ya sera ya fedha ili kuongeza ukuaji wa uchumi.

Bei za bidhaa katika soko la dunia zinatarajiwa kuwa na mwelekeo tofauti. Mathalani, bei ya dhahabu inatarajiwa kuendelea kuongezeka kwa kasi, huku bei ya mafuta ghafi ikitarajiwa kubaki imara. Bei ya

dhahabu inatarajiwa kuongezeka na kufikia zaidi ya dola za Marekani 5,000 kwa wakia kutokana na kuhitajiwa kama akiba ambayo ni salama zaidi. Bei ya mafuta inatarajiwa kuwa kati ya dola za Marekani 62-65 kwa pipa, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na kupungua kwa mahitaji. Mwenendo huo wa bei ya mafuta katika soko la dunia unatarajiwa kupunguza mfumuko wa bei na kuchochea shughuli za uzalishaji nchini.

Uchumi wa ndani

Tathmini iliyofanyika na Benki Kuu mwezi Januari 2026 inaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya uchumi na biashara nchini. Tathmini hiyo imezingatia viashiria mbalimbali vya mwenendo wa uchumi, pamoja na matokeo ya tafiti zilizofanywa na Benki Kuu mwezi Desemba 2025, ikiwemo utafiti kuhusu *Mtazamo wa Mwenendo wa Masoko ya Fedha (Market Perception Survey) na Mtazamo wa Watendaji Wakuu wa Taasisi Kuhusu Mwenendo wa Uchumi (CEOs Economic Perception Survey)*. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi unatarajiwa kukua kwa zaidi ya asilimia 6 katika nusu ya pili ya mwaka 2025/26, ukichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, madini, na ujenzi. Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 7, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, utalii, na viwanda. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la wigo wa asilimia 3 hadi 5, kutokana utulivu wa bei za chakula, kuimarika kwa thamani ya shilingi pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mwelekeo wa Sera ya Fedha kwa nusu ya pili ya mwaka 2025/26

Kwa kuzingatia kuwa mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, Benki Kuu itaendelea na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika nusu ya pili ya mwaka 2025/26. Kwa muktadha huu, katika kikao chake cha Januari 2026, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) iliamua kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR) kiendelee kuwa asilimia 5.75 kwa robo ya mwaka inayoishia

Machi 2026 ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Kikao kijacho cha Kamati ya Sera ya Fedha kinatarajiwa kufanyika mwezi Aprili 2026 ili kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu kitakachotumika katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026. Katika kutekeleza sera ya fedha, Benki Kuu itahakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa CBR.

Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho yanayolenga kuongeza ufanisi katika soko la fedha baina ya benki na kutoa elimu kwa wadau ili kuongeza uelewa kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu. Sambamba na hayo, Benki Kuu itaendelea kuhimiza matumizi ya huduma za malipo ya kidijitali na kuendelea kuhakikisha wananchi wanafuata miongozo na kanuni zinazowataka kutumia shilingi katika kufanya miamala nchini. Vilevile, viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa na nguvu za soko, huku kiwango cha Riba ya Benki Kuu kikitumika kama msingi wa upangaji wa viwango vya riba za mikopo na huduma nyingine za kifedha nchini. Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha katika kutekeleza mikakati ya kutoa elimu ya fedha, kuongeza ujumuishi wa huduma za kifedha nchini pamoja na kumlinda mlaji.

Thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni itaendelea kuamuliwa na nguvu za soko, na hivyo kuukinga uchumi dhidi ya athari zitokanazo na mitikisiko ya uchumi duniani. Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni kwa kuzingatia Sera ya Ushiriki katika soko la fedha za kigeni, ili kupunguza mabadiliko makubwa ya muda mfupi katika kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni, kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuchangia utekelezaji wa sera ya fedha. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha kuwa akiba ya fedha za kigeni inaendelea kuwa ya kutosha, na kanuni na miongozo ya fedha za kigeni inazingatiwa.

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mwezi Juni 2025, Benki Kuu ilitoa Tamko la Sera ya Fedha linaloainisha mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26. Tamko hilo lilizingatia maoteo ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na vihatarishi vyake. Kwa kuzingatia maoteo ambayo yalionesha mfumuko wa bei kuendelea kubakia ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, Benki Kuu ilipanga kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi ili kuwezesha ukuaji wa uchumi, kufikia asilimia 6 kwa Tanzania Bara na asilimia 6.5 kwa Zanzibar kwa mwaka 2025.

Kwa muktadha huo, Tamko la Sera ya Fedha, Mapitio ya Nusu Mwaka wa 2025/26, linatoa tathmini ya utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Vilevile, Tamko hili linaainisha mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, na kutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika nusu ya pili ya mwaka 2025/26 ili kuendelea kuwa na utulivu wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi nchini.

Pamoja na sehemu hii ya utangulizi, Tamko hili limegawanyika kwa mtiririko ufuatao: Sehemu ya pili inaainisha utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Sehemu ya tatu inatoa muhtasari wa mwenendo wa uchumi wa dunia. Sehemu ya nne inatathmini mwenendo wa uchumi hapa nchini. Sehemu ya tano inatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Sehemu ya sita inahitimisha kwa kutoa mwelekeo wa sera ya fedha kwa nusu ya pili ya mwaka 2025/26.

Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu ya Tanzania ina jukumu la kuandaa na kutekeleza sera ya fedha, ikiwa ni moja kati ya majukumu yake. Malengo ya sera ya fedha ni kudumisha utulivu wa bei, ikimaanisha ni kuwa na mfumuko wa bei mdogo na usiobadilika mara kwa mara katika kipindi husika, pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi. Mfumuko wa bei hupimwa kwa kutumia badiliko la mwaka la fahirisi za bei za walaji (CPI), na huwasilishwa kwa asilimia. Lengo la mfumuko wa bei la muda wa kati (hadi miaka 5), ni kati ya asilimia 3 hadi 5.

Ili kutimiza malengo haya, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) hutathmini mwenendo na matarajio ya uchumi na kuamua kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR) kinachoendana na mfumuko wa bei ulio chini na thabiti na kuweka mazingira ya kuchochea ukuaji wa uchumi. Benki Kuu ya Tanzania hutekeleza sera ya fedha kwa kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki ambayo ni kiashiria cha utekelezaji wa sera ya fedha kinakuwa ndani ya wigo wa CBR.

Ili kuoanisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki na CBR, Benki hutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha. Nyenzo hizi ni pamoja na mikopo ya muda mfupi (repo na reverse repo), dhamana za Serikali za siku 35 na 91, kuongeza au kupunguza kiwango cha amana kinachotakiwa kuweka kisheria na benki katika Benki Kuu (SMR), pamoja na mauzo au manunuzi ya fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni. Vilevile, Benki hutumia nyenzo nyingine ambazo ni mikopo ya siku moja na ile inayolipwa ndani ya siku husika, ambayo hutolewa kwa benki zenye uhitaji ili kuhakikisha kuwa mifumo ya malipo inafanya kazi kwa ufanisi.

Katika kutekeleza sera ya fedha, Benki huzingatia uwazi katika maamuzi yake. Maamuzi ya MPC, yakiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu, huwasilishwa kwa benki kupitia mikutano ya Gavana na watendaji wakuu wa benki, na kwa umma kupitia vyombo vya habari. Aidha, Benki huchapisha matamko ya Kamati ya Sera ya fedha, Ripoti ya Sera ya Fedha, pamoja na ripoti nyingine ambazo huainisha matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha, mwelekeo wa sera ya fedha, maamuzi CBR na mwendendo wa uchumi kwa ujumla. Ripoti hizi zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania (www.bot.go.tz).

Msingi wa kisheria wa Sera ya Fedha

i. Mwanzo wa kila mwaka wa fedha, Benki Kuu ya Tanzania hutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika Tamko lake la Sera ya Fedha kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.

ii. Tamko la Sera ya Fedha huidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania na kuwasilishwa bungeni kupitia kwa Waziri anayesimamia masuala ya fedha kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Benki Kuu, Sura Na. 197.

iii. Utaratibu huo pia unafuatwa wakati wa uandaaji wa Mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, ambayo huainisha maendeleo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo yake, matarajio kwa kipindi cha mwaka kilichosalia, na hatua zitakazochukuliwa ili kufikia malengo ya sera.

iv. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu, ambayo inaongozwa na Gavana, inawajibika kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kila robo mwaka, kuendana na malengo ya sera za uchumi za Serikali.

v. Kamati ya Ufuatiliaji na Uangalizi ya Menejimenti ya Benki Kuu inakutana kila siku kutathmini mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki (kiashiria cha uendeshaji) na kuamua hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha riba hiyo inabaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu.

SEHEMU YA PILI

2.0 MSIMAMO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA

2.1 Msimamo wa sera ya fedha

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, sera ya fedha ililenga kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya wigo wa asilimia 3 hadi 5 na kuwezesha ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 6 kwa Tanzania Bara, na asilimia 6.5 kwa Zanzibar katika 2025. Hivyo, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilifanya mikutano yake ya kila robo mwaka, mwezi Julai na Oktoba 2025, kwa lengo la kutathmini mwenendo na matarajio ya uchumi wa dunia na hapa nchini, ili kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kinachohitajika kufikia malengo hayo.

Katika mkutano wake uliofanyika Julai 2025, MPC ilipunguza kiwango cha CBR kutoka asilimia 6 hadi asilimia 5.75 kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2025. Uamuzi huo ulitokana na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Hali hii ilitokana na uwepo wa chakula cha kutosha nchini, utulivu wa thamani ya shilingi, na kuimarika kwa mazingira ya uchumi wa dunia ambayo yalitegemewa kuwezesha kuwa na mfumuko wa bei mdogo nchini. Shughuli za uchumi zilitarajiwa kuendelea kukua kwa kasi, kutokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara, uthabiti wa sekta ya fedha, na ongezeko la mahitaji ya mikopo kwa sekta binafsi. Katika mkutano wa Oktoba 2025, MPC iliamua CBR kuendelea kuwa asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2025, kutokana na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi.

2.2 Utekelezaji wa sera ya fedha

Utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha ukwasi katika benki za biashara unaendelea kuwa wa kutosha na riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki (*7-day interbank rate*) inabaki ndani ya wigo wa asilimia ± 2 ya CBR. Katika kufikia malengo hayo, Benki Kuu iliongeza ukwasi katika benki za biashara kwa kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha, hususan kutoa mikopo ya muda mfupi (*reverse repurchase agreements*). Benki Kuu pia ilitumia nyenzo za kupunguza ukwasi kwa kuuza dhamana za muda mfupi (*repurchase agreements*) na dhamana za Serikali za muda mfupi ili kupunguza kiwango cha ukwasi pale ilipohitajika[1]. Vilevile, Benki ilinunua na kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni ili kupunguza au kuongeza kiwango cha ukwasi, sambamba na lengo la kuhakikisha utulivu katika soko la fedha za kigeni.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulihakikisha upatikanaji wa ukwasi wa kutosha katika soko la fedha baina ya benki, sambamba na mahitaji ya shughuli za uchumi. Kiwango cha ukwasi kiliongezeka, sanjari na ongezeko la amana za benki za biashara (Kielelezo 2.1). Kuongezeka kwa ukwasi kuliimarisha uwezo wa benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi, na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi. Riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki ilibaki ndani ya wigo wa asilimia ±2 ya CBR (Kielelezo 2.2). Mwenendo huu unaashiria uwezo wa Benki Kuu katika kudhibiti viwango vya riba vya muda mfupi, ili kufikia malengo ya mfumuko wa bei na kusaidia ukuaji wa uchumi.

[1] Dhamana za siku 91 na siku 35 hutumika zaidi katika utekelezaji wa sera ya fedha hususan pale Benki Kuu inapotaka kupunguza kiwango cha ukwasi kwenye uchumi.

Kielelezo 2.1: Amana za Mabenki



Chanzo: Benki kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7



Chanzo: Benki kuu ya Tanzania

SEHEMU YA TATU

3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA

3.1 Mwenendo wa shughuli za uzalishaji

Uchumi wa dunia umeendelea kuwa imara licha ya ongezeko la vikwazo vya biashara, mivutano ya kisiasa na kutotabirika kwa sera za kiuchumi. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji, uwekezaji, na hatua nzuri zilizofikiwa katika majadiliano ya kupunguza ushuru wa forodha, pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi. Kutokana na mwenendo huu wa kuridhisha, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2026, lilifanya maboresho ya makadirio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 kutoka asilimia 3.2 hadi kufikia asilimia 3.3 [2]. Katika nchi zilizoendelea, ukuaji unakadiriwa kufikia asilimia 1.7, ambapo uchumi wa Marekani unatarajiwa kukua kwa asilimia 2.1, kutokana na uwekezaji mkubwa katika teknolojia. Ukuaji katika eneo la Ulaya unatarajiwa kuwa wa wastani, kwa asilimia 1.4, ukichangiwa na ongezeko la matumizi ya serikali (Jedwali 3.1). Kwa upande wa nchi zinazoibukia kiuchumi, India inatarajiwa kukua kwa kasi kutokana uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu na ukuaji wa sekta ya tehama. Nchini China, uchumi unatarajiwa kukua kwa kasi kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye teknolojia. Ukuaji wa uchumi kwa ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara pia unatarajiwa kuendelea kuwa imara.

[2] Taarifa ya mwelekeo wa uchumi wa dunia ya mwezi Januari 2026.

Jedwali 3.1: Ukuaji wa Pato la Taifa

Asilimia

	Halisi						Makadirio					
	IMF	OECD	Benki ya Dunia	IMF	OECD	Benki ya Dunia	IMF	OECD	Benki ya Dunia	IMF	OECD	Benki ya Dunia
	2023			2024			2025			2026		
Dunia	3.0	2.9	2.1	3.3	3.2	2.7	3.3	3.1	2.7	3.3	2.9	2.4
Nchi zilizoendelea	1.5	n.a	0.7	1.8	n.a	1.7	1.7	n.a	1.7	1.8	n.a	1.4
Marekani	2.1	2.4	1.1	2.8	2.8	2.8	2.1	2.2	2.3	2.4	1.7	1.6
Eneo la Ulaya	0.7	0.6	1.3	0.9	0.7	0.7	1.4	1.0	1.0	1.3	1.2	0.8
Uingereza	0.5	n.a	n.a	1.1	0.9	n.a	1.4	1.4	n.a	1.3	1.2	n.a
Japani	2.0	1.7	0.8	0.1	0.1	0.0	1.1	1.1	0.9	0.7	0.9	0.8
Nchi zinazoibukia na Kuendelea Kiuchumi	4.0	n.a	4.0	4.3	n.a	4.1	4.4	n.a	4.1	4.2	n.a	3.8
Brazili	3.0	3.0	1.2	3.4	3.4	3.2	2.5	2.1	2.2	1.6	1.7	2.2
Urusi	2.2	n.a	n.a	4.1	4.1	3.4	0.6	1.3	1.6	0.8	0.9	1.2
India	6.3	6.3	6.3	6.5	6.3	6.5	7.3	6.4	6.7	6.4	6.2	6.5
China	5.0	5.2	5.6	5.0	5.0	4.9	5.0	4.1	4.5	4.5	4.4	4.0
Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara	3.3	n.a	3.2	4.0	n.a	3.2	4.4	n.a	4.1	4.6	n.a	4.1

Chanzo: Ripoti ya IMF ya Mwelekeo wa uchumi, Januari 2026, Ripoti ya Benki ya dunia kuhusu matarajio ya Uchumi wa dunia, Januari 2026 na Ripoti ya Mwelekeo wa uchumi ya OECD, Desemba 2024.
Tanbihi: inamaanisha kuwa takwimu haipo kwa muda ambao repoti hii inaandaliwa

3.2 Mfumuko wa bei

Katika nusu ya kwanza ya 2025/26, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi na kufikia au kuwa chini ya malengo ya benki kuu nyingi duniani, kutokana na kushuka kwa bei za mafuta ghafi na matokeo ya utekelezaji wa sera za fedha iliyolenga kupunguza ukwasi katika uchumi (Kielelezo 3.1a). Kufuatia mwenendo huu wa mfumuko wa bei, benki kuu nyingi ziliamua kutokubadili au kushusha viwango vyao vya riba za sera ya fedha ili kuchagiza ukuaji wa uchumi.

Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei ulipungua na kukaribia lengo la asilimia mbili, huku kasi ya kupungua kwa mfumuko wa bei ikiwa ndogo katika nchi zilizoathiriwa zaidi na ongezeko la ushuru wa forodha (Kielelezo 3.1a). Kadhalika, katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, hususan nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), mfumuko wa bei ulikuwa ndani ya malengo ya mtangamano wa kiuchumi (Kielelezo 3.1b na 3.1c). Mwenendo huu ulitokana na utekelezaji wa sera ya fedha, pamoja na mfumuko mdogo wa bei katika nchi washirika wa biashara na utulivu wa bei za chakula.

Kielelezo 3.1a: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Asilimia



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi husika

Kielelezo 3.1b: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za EAC

Asilimia



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi husika

Kielelezo 3.1c: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC

Asilimia



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi husika

3.3 Mwenendo wa bei za bidhaa

Bei za bidhaa katika soko la dunia zilibadilika kwa kiasi kikubwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Bei za mafuta ghafi iliendelea kushuka, na kufikia wastani wa dola za Marekani 64.8 kwa pipa, kutokana na ongezeko la uzalishaji na kupungua kwa mahitaji (Kielelezo 3.2a). Kupungua kwa bei za mafuta kulileta unafuu kwenye mfumuko wa bei nchini, kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni na shinikizo kwenye thamani ya shilingi, ikizingatiwa kuwa uagizaji wa mafuta huchukua takriban asilimia 17 ya thamani ya bidhaa zote zinazoagizwa toka nje

ya nchi. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu, ikifikia dola za Marekani 4,309.2 kwa wakia, kutokana na ongezeko la mahitaji kwa ajili ya uwekezaji (kuweka akiba) pamoja na ununuzi unaofanywa na benki kuu duniani. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kulichangia kuimarika kwa mapato ya fedha za kigeni nchini, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, pamoja na kuimarisha thamani ya shilingi.

Bei za mazao zilikuwa na mienendo tofauti kutegemea hali ya mahitaji na upatikanaji. Bei ya kahawa ilipungua, ambapo bei ya Arabika ilishuka hadi dola za Marekani 8.2 kwa kilo huku bei ya Robusta ikishuka hadi dola za Marekani 4.2 kwa kilo, kutokana na ongezeko la uzalishaji katika nchi zinazozalisha kahawa kwa wingi kama Brazil na Vietnam. Bei ya sukari ilishuka hadi dola za Marekani 320 kwa tani, kufuatia ongezeko la uzalishaji hususan kutoka India na Thailand. Vilevile, bei ya pamba ilishuka kutokana na kupungua kwa mahitaji katika masoko ya kimataifa na matarajio ya kuongezeka kwa uzalishaji. Wakati huohuo, bei ya mchele iliongezeka hadi dola za Marekani 424 kwa tani, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, hususan kutoka China (Kielelezo 3.2b).

Kielelezo 3.2a: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia



Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects na Bloomberg

Kielelezo 3.2b: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia



Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects na Bloomberg

3.4 Mwenendo wa masoko ya fedha duniani

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, riba za hati fungani za serikali zilikuwa na mienendo tofauti katika masoko ya fedha duniani. Mwenendo huu uliakisi mabadiliko ya mfumuko wa bei, ukuaji wa uchumi, masoko ya ajira, na matarajio ya sera za fedha na kibajeti. Nchini Marekani, riba za hati fungani za serikali zilipungua hususan zile za muda mfupi. Katika nchi za Umoja wa Ulaya, riba za hati fungani ziliongezeka, huku nchini Uingereza, riba zikipungua kutokana na kushuka kwa mfumuko wa bei pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi, huku Benki Kuu ya Uingereza ikishusha riba ya sera ya fedha kwa asilimia 0.25. Nchini China, riba za hati fungani za muda mfupi hazikuwa na mabadiliko makubwa wakati zile za muda wa kati na muda mrefu zikiongezeka. Aidha, riba za hati fungani ziliongezeka nchini Australia.

SEHEMU YA NNE

4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI

4.1 Pato la Taifa

Uchumi uliendelea kuimarika katika robo tatu za kwanza za mwaka 2025. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 6, ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 4.1a na 4.1b). Ukuaji huo ulichagizwa zaidi na uwekezaji wa sekta binafsi na umma, sambamba na maboresho yanayoendelea kufanyika katika utekelezaji wa sera nchini, pamoja na kuimarika kwa mazingira ya uchumi duniani. Uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.9, ikiwa karibu sawa na makadirio ya awali ya asilimia 6 na zaidi ya ukuaji wa asilimia 5.5 katika mwaka 2024. Mwenendo huo unatokana na ukuaji wa asilimia 6 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2025 na kuimarika kwa shughuli za uchumi na biashara katika robo ya nne. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, na uchimbaji madini na mawe.

Kielelezo 4.1a: Ukuaji wa Pato la Taifa (Jan – Septemba 2025).



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 4.1b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa (Jan – Septemba 2025).

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ukuaji wa uchumi wa Zanzibar pia uliendelea kuwa imara, ukichangiwa na maboresho yanayoendelea kufanywa kwenye miundombinu, uzalishaji viwandani na sekta ya utalii. Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2025, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 7 katika kipindi kama hicho cha mwaka (Kielelezo 4.2a na 4.2b).

Kielelezo 4.2a: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa kwa Zanzibar



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

Kielelezo 4.2b: Mchango wa wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi Katika Pato la Taifa kwa Zanzibar



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

4.2 Mfumuko wa Bei

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, na malengo ya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za EAC na SADC ya kiwango kisichozidi asilimia 8 na asilimia 3 hadi 7, mtawalia (Kielelezo 4.3a). Mathalani, mfumuko wa bei ulikuwa kati ya asilimia 3.1 hadi asilimia 3.6, ikiwa ni wastani wa asilimia 3.5, ikilinganishwa na asilimia 3.1 kwa mwaka uliotangulia (Kielelezo 4.3b). Kiwango hicho kidogo cha mfumuko wa bei kilitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, uimara wa thamani ya shilingi, na kupungua kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia. Mfumuko wa bei za chakula katika kipindi hicho uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.2, kutoka asilimia 2.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei za msingi (*core inflation*) ambao huchangia takriban asilimia 73.9 ya kapu la walaji ulipungua hadi wastani wa asilimia 2.1 kutoka asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mfumuko wa bei wa jumla (Kielelezo 4.3c).

Kielelezo 4.3a: Mfumuko wa Bei na Malengo ya Nchi na Kikanda



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 4.3b: Mfumuko wa Bei



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 4.3c: Mchango Katika Mfumuko wa Bei

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Mfumuko wa bei kwa upande wa Zanzibar, ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.7 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (Kielelezo 4.4 na Jedwali 4.1). Mfumuko wa bei za chakula ulipungua hadi ulifikia wastani wa asilimia 4.8, ukilinganishwa na wastani wa asilimia 8, kufuatia kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani, sambamba na kuimarika kwa thamani ya shilingi. Kupungua kwa bei za vyakula kulichangiwa pia na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo kupunguza ushuru wa bidhaa za chakula zinazoagizwa toka nje ya nchi na tozo za bandari (wharfage), misamaha ya gharama za kuhifadhi bidhaa za chakula, pamoja na kuhamasisha uagizaji wa chakula moja kwa moja kupitia bandari za ndani. Mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za chakula ulipungua kidogo hadi wastani wa 2.7, kutoka asilimia 2.8, kutokana na kupungua kwa bei za nishati katika soko la dunia.

Kielelezo 4.4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

Jedwali 4.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar

Asilimia

		Badiliko kila Mwezi			Badiliko kila Mwaka		
Makundi ya msingi	Uzito	Dec-24	Nov-25	Dec-25	Dec-24	Nov-25	Dec-25
Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kileo	41.9	1.1	-2.7	2.0	7.9	5.3	6.2
Vinywaji vyenye Vileo, Tumbaku na Madawa ya binadamu	0.2	-8.3	1.8	-1.5	15.4	3.3	10.9
Mavazi na Viatu	6.3	1.4	-0.2	0.2	2.0	5.3	4.0
Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyingine	25.8	-1.1	0.8	-0.5	2.8	0.0	0.6
Samani, Vifaa vya Nyumbani na Matengenezo ya Kawaida ya Nyumba	4.8	0.3	0.1	0.3	1.7	2.7	2.7
Afya	1.3	0.0	0.7	0.1	-2.4	2.1	2.2
Uchukuzi	9.1	-0.1	0.4	-0.4	1.2	3.4	3.1
Taarifa na mawasiliano	4.2	0.7	0.0	0.1	3.5	0.7	0.1
Burudani, Michezo na Utamaduni	1.1	2.1	0.7	1.1	4.9	6.4	5.3
Elimu	1.6	0.0	-0.2	0.3	2.8	0.8	1.1
Huduma za Migahawa na Malazi	1.4	0.0	0.0	0.4	13.7	1.9	2.2
Bima na Huduma za Fedha	0.5	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Huduma binafsi, Ulinzi wa Kijamii na Bidhaa na Huduma Mbalimbali	1.7	0.0	-0.3	0.2	0.8	4.5	4.8
Mfumuko wa bei wa jumla	100.0	0.4	-1.0	0.8	4.9	3.3	3.8
Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula	41.9	1.2	-2.8	2.0	8.1	4.5	5.4
Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula	58.6	-0.3	0.4	-0.1	2.5	2.4	2.5

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

4.3 Viwango vya Riba

Viwango vya riba za mikopo na amana viliendelea kuwa tulivu. Riba za mikopo zilikuwa takribani asilimia 15, wakati riba za mikopo ya wateja wakubwa na wale wanaoaminika zaidi (*negotiated lending rates*) zilikuwa asilimia 13. Riba za amana zilikuwa wastani wa takribani asilimia 9, huku riba za amana za wateja wakubwa zikiwa asilimia 11 (Kielelezo 4.5a). Wakati huo huo, riba za dhamana za Serikali zilipungua, sanjari na ongezeko la mahitaji ya uwekezaji katika dhamana za Serikali (Kielelezo 4.5b).

Kielelezo 4.5a: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa Benki za Biashara



Chanzo: Mabenki na Benki kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.5b: Riba Katika Masoko ya Fedha



Chanzo: Mabenki na Benki kuu ya Tanzania

4.4 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi

Ujazi wa fedha uliendelea kukua sanjari na sera wezeshi ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 21.8 katika nusu ya kwanza ya 2025/26, ukichangiwa zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, ambayo ilikuwa kwa asilimia 17.6, ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 16.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (Kielelezo 4.6a na 4.6b). Ukuaji huu wa mikopo kwa sekta binafsi unaakisi kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na sera wezeshi ya fedha. Vilevile, ukuaji huu ulisaidiwa na utekelezaji wa hatua za kisera zilizolenga kuongeza upatikanaji wa mikopo, kupitia mfuko wa udhamini wa mikopo na mkopo maalumu wa Benki Kuu kwa lengo la kuongeza utoaji wa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

Kielelezo 4.6a: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.6b: Mchango wa Ukuaji wa M3



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Shughuli zote za kiuchumi zilikuwa na ongezeko la ukuaji wa mikopo, ambapo mikopo kwa shughuli binafsi ambazo kwa kiasi kikubwa huelekezwa kwenye biashara ndogo na za kati (SMEs) iliendelea kuwa kichocheo kikuu cha ukuaji, ikifuatiwa na shughuli za biashara na kilimo (Kielelezo 4.7a). Ukuaji wa mikopo kwa shughuli za kilimo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na fedha zilizotolewa na Benki Kuu kupitia mkopo maalum wa Shilingi trilioni 1 pamoja na unafuu unaotolewa kwenye amana za benki zinazotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu, ambazo kwa pamoja zimeongeza upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima na biashara za kilimo. Mikopo kwa shughuli binafsi iliendelea kuchukua sehemu kubwa zaidi ya mikopo yote kwa asilimia 36, ikifuatiwa na sekta ya biashara kwa asilimia 15.3 na kilimo kwa asilimia 13.2 (Kielelezo 4.7b).

Kielelezo 4.7a Mchango wa Shughuli za Uchumi Katika Ukuaji wa Mikopo, kwa Asilimia



Chanzo: Mabenki na Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.7b: Mgawanyo wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi, kwa Asilimia



Chanzo: Mabenki na Benki Kuu ya Tanzania

4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Sera ya bajeti iliendelea kujikita katika kuongeza ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato, na kupanga matumizi kuendana na upatikanaji wa mapato. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa Tanzania bara ulikuwa wa kuridhisha, ambapo mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 20,303 (Kielelezo 4.8a). Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 16,908.2, yakivuka lengo kwa asilimia 3, kutokana na kuimarika kwa usimamizi wa kodi pamoja na utayari wa kulipa kodi kwa hiyari. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 3,394.8 sawa na asilimia 83 ya lengo. Wakati huohuo, matumizi ya Serikali yalikuwa Shilingi bilioni 24,324.6, ambapo matumizi ya kugharamia shughuli za maendeleo yalikuwa ni asilimia 38.8.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ulikuwa wa kuridhisha. Jumla ya mapato ya ndani na misaada ilifikia shilingi bilioni 1,186.6, juu ya lengo kwa asilimia 1.9. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 1,079.8, sawa na asilimia 96.2 ya lengo, huku misaada ikifikia shilingi bilioni 106.7, zaidi ya mara mbili ya lengo. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 972.6, sawa na asilimia 99.2 ya lengo, huku makundi yote ya kodi yakivuka lengo, isipokuwa kodi ya mapato (*Income Tax*) na kodi nyinginezo (*Other taxes*). Mapato yasiyo ya kodi yalikuwa asilimia 75.4 ya lengo (Kielelezo 4.8b). Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi 1,905.8 bilioni, ambapo matumizi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo yalikuwa takriban nusu ya matumizi yote (Kielelezo 4.8c).

Kielelezo 4.8a: Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Shilingi bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.8b : Mapato ya Serikali ya Zanzibar

Shilingi bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania.

Kielelezo 4.8c : Matumizi ya Serikali ya Zanzibar

Shilingi bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania.

4.6 Deni la Serikali

Deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu ambapo uwiano wa thamani ya sasa (*Present Value*) wa deni la serikali kwa Pato la Taifa (GDP) umepungua na kufikia asilimia 40.7 kutoka asilimia 41.1 kwa mwaka uliotangulia. Kiwango hiki kilikuwa chini ya ukomo wa uhimilivu wa deni wa asilimia 55 na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Afrika Mashariki (EAC) cha ukomo wa asilimia 50 ya Pato la Taifa (Jedwali 4.2). Kwa thamani ya kawaida, deni hili lilikuwa asilimia 49 ya pato la taifa, chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za SADC cha ukomo wa asilimia 60.

Deni la Serikali, likijumisha deni la ndani na la nje, lilifikia dola za Marekani milioni 44,721.3 mwishoni mwa Desemba 2025. Katika kiasi hicho, deni la nje lilikuwa asilimia 65.9, ambapo kiasi kikubwa ilikuwa ni mikopo nafuu kutoka mashirika ya kimataifa, ikifuatiwa na mikopo ya kibiashara. Kwa kiasi kikubwa, mikopo kutoka nje ya nchi ilitumika kwa ajili ya kugharamia urari wa malipo na bajeti ya serikali, ikifuatiwa na shughuli za usafirishaji na mawasiliano (Jedwali 4.3a, 4.3b, na 4.3c). Deni la ndani la serikali lilifikia shilingi bilioni 37,899 mwezi Desemba 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.7 kutoka mwezi Juni 2025. Ongezeko hili lilitokana na mauzo ya hati fungani za serikali zilizoongeza deni la ndani kwa shilingi bilioni 2,942.8 (Jedwali 4.3d). Kwa upande wa Zanzibar, deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 54.7 hadi kufikia shilingi bilioni 2,385.4. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo viwanja vya ndege, ujenzi wa uwanja wa mpira kwa ajili mashindano ya AFCON, pamoja na miradi ya inayohusiana na utelekezaji wa uchumi wa bluu.

Jedwali 4.2: Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali kwa Mwaka 2025

	Ukomo	2024/25*	2025/26	2026/27	2027/28	2035/36
Uhimilivu deni la umma						
Uwiano wa deni halisi kwa pato la taifa	55	40.7	39.6	38.6	36.9	34.7
Uwiano wa deni halisi kwa mapato	N/A	254.7	233.4	225.6	214.8	205.8
Uwiano wa malipo ya deni kwa mapato	N/A	35.0	45.2	32.9	34.1	31.2
Uhimilivu deni la nje						
Uwiano wa deni halisi kwa pato la taifa	40	24.9	24.4	23.6	22.4	18.0
Uwiano wa deni halisi kwa mauzo ya nje	180	125.4	123.1	123.8	119.3	103.0
Uwiano wa malipo ya deni kwa mauzo ya nje	15	11.6	12.8	12.2	13.7	10.2
Uwiano wa malipo ya deni kwa mapato	18	14.7	15.4	13.8	15.1	10.6

Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi:(*) inamanisha takwimu halisi mpaka kufikia mwisho wa Juni 2025

Jedwali 4.3a: Mwenendo wa Deni

Dola za Marekani Milioni

	Des-24	Jun-25	Des-25[p]
Deni la serikali kuu	39,510.7	41,874.7	44,717.6
Deni la nje la serikali kuu	25,877.1	28,243.6	29,232.6
Asilimia ya deni la nje la serikali kuu	65.5	67.4	65.4
Deni la ndani la serikali kuu	13,633.7	13,631.1	15,485.0
Deni la nje la sekta binafsi	6,116.3	6,517.9	6,072.9
Deni la nje la mashirika ya umma	3.8	3.8	3.8
Jumla ya deni la nje	31,997.1	34,765.3	35,309.2
Deni la taifa	45,630.8	48,396.3	50,794.2

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Jedwali 4.3b: Wakopeshaji wa Deni la Nje

*Dola za Marekani Milioni**

	Des-24		Jun-25		Des-25[p]	
Mkopeshaji	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Mashirika ya fedha ya kimataifa	18,145.8	56.7	19,756.7	56.8	20,544.3	58.2
Deni ambalo halijalipwa	18,114.9	56.6	19,721.2	56.7	20,507.4	58.1
Malimbikizo ya riba	30.9	0.1	35.5	0.1	37.0	0.1
Nchi washirika wa maendeleo	1,270.3	4.0	1,507.8	4.3	1,513.5	4.3
Deni ambalo halijalipwa	1,193.2	3.7	1,429.1	4.1	1,433.4	4.1
Malimbikizo ya riba	77.2	0.2	78.7	0.2	80.1	0.2
Benki za kimataifa za biashara	11,459.7	35.8	12,439.1	35.8	12,538.0	35.5
Deni ambalo halijalipwa	11,111.6	34.7	12,024.9	34.6	12,201.8	34.6
Malimbikizo ya riba	348.1	1.1	414.2	1.2	336.2	1.0
Mikopo ya mauzo ya nje	1,121.3	3.5	1,061.7	3.1	713.4	2.0
Deni ambalo halijalipwa	950.1	3.0	877.8	2.5	664.4	1.9
Malimbikizo ya riba	171.2	0.5	183.9	0.5	49.0	0.1
Jumla ya deni la nje	31,997.1	100.0	34,765.3	100.0	35,309.2	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali;
*Takwimu zinajumuisha deni la nje la serikali na la sekta binafsi.

Jedwali 4.3c: Matumizi ya Mikopo ya Nje Iliyopokelewa

Dola za Marekani Milioni

	Des-24		Jun-25		Des-25[p]	
Shughuli ya uchumi	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango(%)
Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support)	6,396.2	24.8	7,454.4	26.5	7,949.8	27.3
Usafirishaji na mawasiliano	5,767.4	22.4	6,279.6	22.3	6,741.0	23.1
Kilimo	1,297.2	5.0	1,537.6	5.5	1,558.8	5.3
Nishati na madini	2,780.5	10.8	2,973.6	10.6	2,945.1	10.1
Viwanda	158.1	0.6	159.6	0.6	157.4	0.5
Huduma za jamii na elimu	6,097.9	23.6	6,586.9	23.4	6,699.0	23.0
Fedha na bima	154.7	0.6	157.9	0.6	163.9	0.6
Utalii	119.8	0.5	121.1	0.4	112.8	0.4
Mali isiyohamishika na ujenzi	1,363.1	5.3	1,308.9	4.6	1,259.2	4.3
Mengineyo	1,665.1	6.5	1,585.3	5.6	1,565.6	5.4
Jumla	25,799.9	100.0	28,164.9	100.0	29,152.5	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Jedwali 4.3d: Deni la Ndani la Serikali

Shilingi bilioni

	Des-25		Jul-25		Des-25^P	
Nyenzo	Kiasi	Asilimia	Kiasi	Asilimia	Kiasi	Asilimia
Dhamana za serikali	28,664.3	87.8	30,170.4	85.0	33,012.5	87.1
Dhamana za serikali za muda mfupi	2,108.0	6.5	2,001.3	5.6	1,951.9	5.2
Hisa za serikali	187.1	0.6	187.1	0.5	135.7	0.4
Dhamana za serikali za muda mrefu	26,369.1	80.8	27,982.0	78.8	30,924.8	81.6
Vyeti vya ushuru	0.1	0.0	0.1	0.0	0.1	0.0
Deni lisilo na dhamana	3,985.0	12.2	5,332.4	15.0	4,886.5	12.9
Madeni mengine*	18.4	0.1	18.4	0.1	0.0	0.0
Bakaa hasi	3,966.6	12.1	5,314.0	15.0	4,886.5	12.9
Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi)	32,649.3	100.0	35,502.8	100.0	37,899.0	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara; na p inamaanisha takwimu za awali

4. 7 Mwenendo wa Urari wa Malipo ya Kawaida

Sekta ya nje iliendelea kuimarika, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilipungua hadi asilimia 2.2 ya Pato la Taifa, ikiwa ni kiwango cha chini zaidi kuwahi kufikiwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, nakisi hii ilipungua hadi dola za Marekani milioni 609.7, kutoka dola za Marekani milioni 657.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mauzo ya nje, hususan dhahabu, utalii, bidhaa za kilimo na usafirishaji (Jedwali 4.4 na Kielezo 4.9). Vilevile, kupungua kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia kulichangia kuimarika kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuendelea kupungua kufuatia jitihada zinazoendelea za kuongeza mapato ya utalii na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, sambamba na bei nzuri ya dhahabu katika soko la dunia.

Jedwali 4.4: Urari wa Malipo ya Kawaida

Dola millioni

	Mwaka			Julai - Desemba	
	2023	2024	2025^p	2024	2025^p
Urari wa bidhaa	-6,032.3	-5,074.0	-4,399.4	-2,096.9	-1,939.8
Zilizouzwa nje*	7,696.6	9,121.6	10,282.4	5,615.7	5,988.7
Zilizonunuliwa nje	-13,728.9	-14,195.6	-14,681.8	-7,712.6	-7,928.5
Urari wa huduma	3,835.9	4,051.7	4,148.5	2,129.9	2,342.4
Mapato	6,231.7	6,846.8	7,290.4	3,760.9	4,014.1
Malipo	-2,395.9	-2,795.0	-3,141.9	-1,631.0	-1,671.7
Urari wa Bidhaa na Huduma	-2,196.5	-1,022.3	-250.9	33.0	402.6
Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje	13,928.3	15,968.4	17,572.7	9,376.6	10,002.8
Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje	-16,124.8	-16,990.7	-17,823.7	-9,343.6	-9,600.2
Urari wa mapato ya vitega uchumi	-1,496.6	-1,887.4	-2,074.3	-998.4	-1,089.1
Yaliyoingia	301.2	311.7	409.6	163.1	236.3
Yaliyotoka	-1,797.7	-2,199.2	-2,483.9	-1,161.4	-1,325.4
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	732.5	529.9	310.0	307.8	76.8
Iliyoingia	1,280.9	1,177.4	878.4	594.4	418.4
ambapo Serikalini	131.0	139.2	32.1	90.1	18.5
Iliyoingia	-548.4	-647.5	-568.3	-286.6	-341.6
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-2,960.6	-2,379.8	-2,015.2	-657.5	-609.7

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Kielelezo 4.9: Urari wa Malipo ya Kawaida

Dola millioni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 6.7 hadi dola za Marekani milioni 10,002.8, kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, kutoka dola za Marekani milioni 9,376.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, utalii, bidhaa za viwandani, na bidhaa za kilimo, hususan tumbaku, korosho, na kahawa na huduma za usafirishaji (Jedwali 4.5 na Kielelezo 4.10). Mauzo ya bidhaa yalifikia dola za Marekani milioni 5,988.7, huku mapato yatokanayo na huduma yakifikia dola za Marekani milioni 4,014.1. Dhahabu na utalii vimeendelea kuwa vyanzo vikuu vya mauzo nje ya nchi, ambapo kwa pamoja vimechangia asilimia 47.7 ya mauzo yote ya bidhaa na huduma. Kwa mwaka 2025, mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 17,599.2, kutoka dola za Marekani milioni 15,968.4 kwa mwaka 2024.

Jedwali 4.5: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

Dola Milioni

	Mwaka			Julai - Desemba	
	2023	2024	2025 p	2024	2025 p
Bidhaa asilia	953.3	1,473.3	1,512.2	1,124.1	1,196.0
Bidhaa zisizo asilia	6,321.6	7,228.8	8,403.2	4,221.4	4,553.1
ambapo Dhahabu	3,058.9	3,419.6	4,697.6	1,934.3	2,582.8
Bidhaa za viwandani	1,363.3	1,341.3	1,548.6	709.4	771.3
Mazao ya mboga na maua	417.2	507.0	479.3	395.8	367.0
Mapato ya huduma	6,231.7	6,846.8	7,316.8	3,760.9	4,014.1
ambapo Utalii	3,373.8	3,903.1	3,948.2	2,180.4	2,200.4
Usafirishaji	2,333.4	2,353.4	2,796.5	1,296.8	1,511.9
Mauzo ya bidhaa na huduma	13,928.3	15,968.4	17,599.2	9,376.6	10,002.8

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Kielelezo 4.10: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

Dola Milioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilifikia dola za Marekani milioni 9,600.2, sawa na ongezeko la asilimia 2.7 kutoka dola za Marekani milioni 9,343.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana na uagizaji wa malighafi za viwandani, vifaa vya usafiri, pamoja na mashine na mitambo, hali inayoakisi utekelezaji wa ajenda ya kuinua uchumi wa viwanda nchini. Vilevile, malipo ya usafirishaji wa mizigo yalichangia ongezeko la malipo ya huduma, huku uagizaji wa bidhaa za petroli, ambazo zilichangia asilimia 17 ya uagizaji wa bidhaa haukuwa na mabadiliko makubwa kufuatia kupungua kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia (Jedwali 4.6). Katika kipindi cha mwaka 2025, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa toka nje ya nchi zilifikia dola za Marekani milioni 17,826.1 mwaka 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,990.7 mwaka 2024.

Jedwali 4.6: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

Dola Milioni

	Mwaka			Julai - Desemba	
	2023	2024	2025p	2024	2025p
Bidhaa za kukuza mtaji	2,893.4	2,971.5	3,316.2	1,679.4	1,934.0
Bidhaa za kati	9,389.1	9,819.9	9,834.0	5,289.7	5,190.1
Malighafi za viwanda	4,307.1	4,641.0	5,156.0	2,579.9	2,661.4
Mafuta na vilainishi	2,915.7	2,784.1	2,418.8	1,398.6	1,349.2
ambapo Bidhaa za petroli zilizochujwa	2,725.8	2,552.3	2,380.1	1,309.1	1,323.8
Bidhaa za matumizi ya kawaida	1,444.2	1,402.1	1,529.4	742.5	803.4
Malipo ya huduma	2,395.9	2,795.0	3,144.4	1,631.0	1,671.7
Usafirishaji	1,326.4	1,411.9	1,436.1	806.9	775.8
Utalii	477.2	522.3	650.4	330.4	342.7
Nyinginezo	592.3	860.9	1,057.9	493.6	553.2
Bidhaa na huduma	16,124.8	16,990.7	17,826.1	9,343.6	9,600.2

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Urari wa malipo ya kawaida waimarika ukichangiwa na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, shughuli za utalii na huduma za usafirishaji

Urari wa malipo ya kawaida umeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni, hususan katika nusu ya pili ya mwaka 2025, ukichangiwa na ongezeko kubwa la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Mauzo ya nje yaliyoongezeka zaidi yalikuwa madini, mazao ya kilimo hasa kahawa, tumbaku na pamba, na huduma za utalii, na usafirishaji. Wakati huo huo, kasi ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje ilipungua, hususan kutokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli.

Kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia kuliimarisha kwa kiasi kikubwa mauzo ya madini nje ya nchi, ambapo katika nusu ya pili ya mwaka 2025, bei ya dhahabu iliongezeka hadi dola 4,309.2 mwezi Desemba 2025, kutoka dola 2,648 mwezi Desemba 2024. Ongezeko hili la bei lilichangia kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu kwa asilimia 36.4 hadi kufikia dola milioni 2,582.8. Wakati huo huo, uagizaji wa bidhaa za mafuta, ambao ulichangia takribani asilimia 17 ya uagizaji wa bidhaa, ulipungua kwa asilimia 14 kutokana na mwenendo mzuri wa bei katika soko la dunia. Aidha, jitihada zinazofanywa na serikali za kuzalisha baadhi ya bidhaa ndani ya nchi badala ya kuagiza kutoka nje hususan sukari, ngano, mafuta ya kula na mbolea zimesaidia kupunguza nakisi ya urari wa malipo ya kawaida, kutoka asilimia 7.1 ya Pato la Taifa mwaka 2022 hadi asilimia 2.2 ya Pato la Taifa mwaka 2025.

Mauzo ya huduma nje ya nchi nayo yalichangia kuimarika kwa urari wa malipo ya kawaida, ikiongozwa na sekta za utalii na usafirishaji. Idadi ya watalii iliongezeka kwa asilimia 8 hadi kufikia watalii 1,297,708, kutoka watalii 1,196,535 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, na hivyo kuongeza mapato ya utalii. Kuimarika kwa shughuli usafirishaji kwenda nchi jirani nako kumechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida.

Matarajio ni nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ikuendelea kupungua kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu hasa katika kipindi hiki ambapo bei kwenye soko la dunia zipo juu, sambamba na matarajio ya kuendelea kuongezeka kwa huduma za utalii na usafirishaji, pamoja na jitihada zinazochukuliwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazoagizwa nje hapa nchini.

Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuimarika sanjari na shughuli za utalii. Urari wa malipo ya kawaida katika nusu ya kwanza ya 2025/26 ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 467.3, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 421 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 889.6 kutoka dola za Marekani milioni 737.4. Mapato ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 20.9 hadi dola za Marekani milioni 862.8 katika kipindi hicho, kutokana na ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 8.7 hadi dola za Marekani milioni 354.1 kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji na bidhaa za walaji (Jedwali 4.7, Kielelezo 4.11a na 4.11b).

Jedwali 4.8: Urari wa Malipo ya Kawaida Zanzibar

Dola milioni

	Mwaka			Julai - Desemba	
	2023	2024	2025^p	2024	2025^p
Bidhaa za kukuza mtaji	2,893.4	2,971.5	3,316.2	1,679.4	1,934.0
Bidhaa za kati	9,389.1	9,819.9	9,834.0	5,289.7	5,190.1
Malighafi za viwanda	4,307.1	4,641.0	5,156.0	2,579.9	2,661.4
Mafuta na vilainishi	2,915.7	2,784.1	2,418.8	1,398.6	1,349.2
ambapo Bidhaa za petroli zilizochujwa	2,725.8	2,552.3	2,380.1	1,309.1	1,323.8
Bidhaa za matumizi ya kawaida	1,444.2	1,402.1	1,529.4	742.5	803.4
Malipo ya huduma	2,395.9	2,795.0	3,144.4	1,631.0	1,671.7
Usafirishaji	1,326.4	1,411.9	1,436.1	806.9	775.8
Utalii	477.2	522.3	650.4	330.4	342.7
Nyinginezo	592.3	860.9	1,057.9	493.6	553.2
Bidhaa na huduma	16,124.8	16,990.7	17,826.1	9,343.6	9,600.2

Chanzo: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Kielelezo 4.11a: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

Dola millioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.11b: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nje

Dola millioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

4.8 Mwenendo wa Ukwasi wa Fedha za Kigeni, Thamani ya Shilingi na Akiba ya Fedha za Kigeni

Soko la fedha za kigeni lilikuwa na ukwasi wa kutosha katika kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26. Mwenendo huu ulichangiwa na ongezeko la mapato kutokana na mauzo ya nje ya nchi, hususan dhahabu, utalii na korosho. Aidha, Benki Kuu ilishiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni katika vipindi vichache, ikiwa ni moja ya nyenzo za utekelezaji wa sera ya fedha na kudumisha utulivu katika soko la fedha za kigeni.

Sambamba na uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi wa fedha za kigeni, Shilingi iliendelea kuimarika. Katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2025/26, thamani ya Shilingi iliimarika kwa asilimia 5.5, ikilinganishwa na kushuka kwa thamani kwa asilimia 7.42 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (Kielelezo 4.12). Aidha, kiwango cha kubadilisha fedha katika soko la rejareja, kiliendana na kile cha ubadilishaji katika soko la jumla (IFEM), hali inayoashiria ongezeko la imani katika soko.

Kielelezo 4.12: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26 ambapo ilifikia dola za Marekani milioni 6,329 mwishoni mwa Desemba 2025, kutoka dola za Marekani milioni 5,971.5 mwishoni mwa Juni 2025, huku sehemu ya dhahabu fedha ikiongezeka kufikia asilimia 13, kutoka asilimia moja. Kiasi hiki kinatosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa angalau miezi 4.9 (Kielelezo 4.13a). Kiwango hiki kinazidi lengo la nchi la angalau miezi 4 na Jumuiya ya Afrika Mashariki la miezi 4.5, na hivyo kutosheleza kuhimili mitikisiko ya kiuchumi toka nje ya nchi (Kielelezo 4.12b). Aidha, akiba ya fedha za kigeni inatarajiwa kuendelea kuwa ya kutosha, ikichangiwa na mpango wa ununuzi wa dhahabu kutoka soko la ndani, mwenendo mzuri wa mauzo ya nje hususan dhahabu na shughuli za utalii.

Kielelezo 4.13a: Akiba ya Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.13b: Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa na Huduma



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, thabiti na himilivu dhidi ya mitikisiko ya muda mfupi na wa kati, huku viashiria vyote vikiwa ndani ya wigo unaokubalika. Sekta ya benki, ambayo inachangia takriban asilimia 70 ya sekta ya fedha, ilikuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha, na yenye kutengeneza faida, huku ikiendelea kunufaika na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma. Uwiano wa mtaji kwa rasilimali (*Common Equity Tier I ratio*) ulikuwa asilimia 18.3, juu ya kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 8.5. Ubora wa rasilimali za benki uliimarika, kufuatia kupungua kwa mikopo chechefu (NPLs) hadi asilimia 2.8 ya mikopo yote mwishoni mwa Desemba 2025 kutoka asilimia 3.3 mwishoni mwa Juni 2025, chini ya kiwango kinachohimilika cha asilimia 5. Mikopo chechefu inatarajiwa kuendelea kupungua, na hivyo kuchagiza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupungua kwa gharama za mikopo.

Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza hatua za kupunguza mikopo chechefu na kuimarisha usimamizi wa vihatarishi katika sekta ya benki kupitia maboresho ya sera na kanuni mbalimbali. Hatua hizo zinajumuisha kufanya usimamizi unaozingatia vihatarishi na kuzitaka benki kuongeza umakini wakati wa kufanya tathmini, utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, Benki Kuu ilianzisha ufuatiliaji maalumu wa mikakati ya kupunguza mikopo chechefu (NPL) katika benki kupitia ukaguzi maalumu, na kuzitaka benki kutumia taarifa kutoka katika kanzidata ya taarifa za wakopaji. Vilevile, benki zimeendelea kuhimizwa kuzingatia kanuni za maadili zilizoandaliwa na Jumuiya ya Mabenki Tanzania (*Tanzania Bankers' Association Code of Conduct*) pamoja na miongozo mingine ili kuimarisha udhibiti wa ndani, na kusaidia kuongeza ubora wa rasilimali.

4.10 Mifumo ya Malipo

Mifumo ya Malipo iliendelea kuwa imara, ikifanya kazi kwa ufanisi, ikiwa na kiwango cha upatikanaji cha asilimia 99.9. Benki Kuu iliendelea kufanya maboresho ya mifumo hii ili kuongeza ufanisi na matumizi. Katika kipindi hiki, Benki ilikamilisha mfumo wa TISS kuhamia katika kiwango cha kimataifa cha ISO 20022, na hivyo kuboresha usimamizi na kuongeza ubora wa taarifa za miamala kupitia mfumo huo. Hatua hii pia itawezesha mfumo wa TISS kusomana na mifumo ya malipo ya kimataifa na kikanda kwa urahisi zaidi hivyo kurahisha uchakataji wa miamala ya kimataifa. Benki pia iliboresha mfumo wa kupokea fedha zinazoingia toka nje ya nchi ili kupunguza gharama za kutuma fedha kutoka kwa watanzania waishio nje ya nchi. Vilevile, Benki Kuu iliendelea kuhimiza utekelezaji wa sheria na kanuni za tozo katika mifumo ya malipo kwa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa maagizo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha mifumo ya malipo inaendelea kuwa salama, nafuu na yenye kuaminika. Jitihada hizi zinalenga kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za malipo za kidijitali nchini.

Mifumo ya malipo ya Afrika Mashariki (EAPS) na ule wa Jumuiya ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SADC-RTGS) iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi katika kuchakata miamala ya nje ya nchi. Ili kuongeza matumizi ya mifumo hii, Benki Kuu kwa kushirikiana na benki kuu za nchi wanachama, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zinazolenga kukabiliana na changamoto zinazopelekea matumizi hafifu ya mifumo hii. Hatua hizi za pamoja na uanzishwaji wa Kamati ya Mifumo ya Malipo (PSC) yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya mifumo ya malipo ya kikanda na ukaguzi wa pamoja wa mifumo ya malipo ili kuongeza mtangamano wa kikanda.

Malipo ya kidijitali yaliendelea kuongezeka, sambamba na ongezeko la matumizi ya Mfumo wa Uhamishaji wa Fedha wa Kielektroniki (Kielelezo 4.14a). Simu za mkononi ziliendelea kuwa nyenzo kuu ya kuwawezesha wananchi wasiofikiwa na huduma za benki kupata huduma mbalimbali za kifedha kwa njia za kidijitali. Kwa kutumia simu za mkononi, wananchi waliweza kupata huduma mbalimbali ikiwemo uhamishaji wa fedha, kwenda ndani na nje ya nchi, kuweka akiba na huduma za mikopo midogo midogo, na huduma ndogondogo za bima. Idadi na thamani ya miamala kupitia simu iliongezeka kwa asilimia 10.2 na 16.5, mtawalia (Kielelezo 4.14b). Aidha, matumizi ya simu katika kufanya miamala yameendelea kuongezeka kufuatia uwepo wa mazingira mazuri ya mifumo ya malipo, gharama nafuu, kuaminika kwa mifumo na watoa huduma, na uwepo miundombinu wezeshi ya kidijitali.

Kielelezo 4.14a: Miamala Katika Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.14b: Malipo Kupitia Simu



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

SEHEMU YA TANO

5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI

5.1 Mwelekeo ya Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia kwa mwaka 2026, unatarajiwa kuendelea kuwa himilivu licha ya vikwazo vya kibiashara na kuongezeka kwa hali ya kutotabirika kwa mazingira ya kiuchumi duniani. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), linakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.3 mwaka 2026, ikiwa ni juu ya makadirio yaliyofanyika mwezi Oktoba kwa asilimia 0.2. Mabadiliko haya kwa kiwango kikubwa yatachangiwa na matarajio ya kukua kwa kasi kwa uchumi wa Marekani na China[3]. Ukuaji wa uchumi katika nchi za Umoja wa Ulaya, unatarajiwa kuimarika kwa wastani, kutokana na kuongezeka kwa matumizi na kupungua kwa mfumuko wa bei. India inatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi kutokana na ongezeko la matumizi na uwekezaji. Kwa ujumla, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani, ambapo kasi ya ukuaji itatofautiana baina ya kanda kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha, maendeleo katika majadiliano kuhusu ushuru wa forodha, na kupungua kwa hali ya kutotabirika kwa sera za kiuchumi. Uchumi wa nchi zilizo kusini mwa jagwa la Sahara unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.6 mwaka 2026, kutoka asilimia 4.4 mwaka 2025 kutokana na maboresho yanayoendelea kufanyika na utekelezaji wa sera zinazolenga kuongeza uthabiti wa uchumi.

Ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) unatarajiwa kuimarika kidogo hadi asilimia 3 kutoka asilimia 2.9 kufuatia maboresho ya kimuundo, ongezeko la uwekezaji katika miundombinu, shughuli za kilimo na nishati, pamoja na jitihada za kuibua

[3] Taarifa ya Mapitio ya Uchumi wa Dunia ya Januari 2026

vyanzo vingine vya uzalishaji mbali na sekta ya madini sambamba na kuimarika kwa mazingira ya uchumi duniani. Kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.2 mwaka 2026, kutoka asilimia 5.6 mwaka 2025 kutokana na matumizi ya serikali katika ujenzi wa miundombinu na ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidigitali.

Mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kuendelea kupungua kwa kasi ndogo katika nusu ya kwanza mwaka 2026. Mfumuko wa bei katika Jumuiya za SADC na EAC, unatarajiwa pia kupungua ukichangiwa na utekelezaji wa sera madhubuti za kiuchumi na kushuka kwa bei ya nishati, hususan mafuta ghafi duniani. Hata hivyo, hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei bado ipo kwa nchi zinazokabiliana na changamoto za kushuka kwa thamani za sarafu zao, upungufu wa chakula, na mazingira magumu ya upatikanaji wa mikopo nje ya nchi. Kwa ujumla hali ya vihatarishi vya kiuchumi duniani inatarajiwa kuendelea kuwa ndogo, japo vinaweza kuathiri mwenendo wa ukuaji wa uchumi hususan kutokana na mivutano ya kiasiasa na kibiashara duniani.

Mwanzoni mwa mwaka 2026, bei za bidhaa katika soko la dunia zinatarajiwa kuwa na mienendo inayotofautiana. Bei ya dhahabu inatarajiwa kuongezeka zaidi na kufikia dola za marekani 5,000 au zaidi kwa wakia ifikapo nusu ya pili ya mwaka 2025/26 kutokana na ongezeko la mahitaji toka benki kuu za nchi mbalimbali. Wakati huohuo, bei za mafuta zinatarajiwa kuwa kati ya dola za Marekani 62-65 kwa pipa kutokana na kupungua kwa mahitaji na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi wazalishaji wa mafuta duniani (OPEC+).

5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani

Mazingira ya kiuchumi nchini yanatarajiwa kuendelea kuchagiza kasi ya ukuaji wa uchumi. Kwa upande wa Tanzania Bara, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia zaidi ya asilimia 6 katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2025/26. Ukuaji huu, utachangiwa zaidi na shughuli za kilimo, madini na ujenzi. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2, ukichangiwa na shughuli za ujenzi, utalii na uzalishaji viwandani. Ukuaji huu utachagizwa pia na uwekezaji unaofanywa na Serikali na sekta binafsi. Vilevile, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unategemewa kuendelea kuchagiza ukuaji wa uchumi katika kipindi kilichosalia cha mwaka 2025/26, kufuatia sera wezeshi ya fedha na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini. Matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia yanatarajiwa pia kuongeza chachu ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi hapa nchini, hususan kupitia ongezeko la mahitaji ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Uwezekano wa kutofikiwa kwa matarajio haya ni mdogo, kutokana na uchumi kutegemea shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Katika nusu ya pili ya mwaka 2025/26, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 kwa Tanzania bara na Zanzibar, ukichangiwa na uwepo wa uhakika wa nishati ya umeme, utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti, pamoja na mfumuko mdogo wa bei kutoka nje ya nchi. Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara unategemewa kuwa kati ya asilimia 3.6 kwa robo ya tatu na asilimia 3.8 kwa robo ya nne ya mwaka 2025/26. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki chini ya asilimia 5. Kwa ujumla, vihatarishi vinavyoweza kusababisha ongezeko la mfumuko wa bei bado vipo chini, japo matarajio ya mvua za chini ya wastani yanaweza kuathiri bei za chakula nchini. Hata hivyo, akiba ya kutosha ya chakula iliyopo katika maghala ya chakula, ya taifa (*NFRA*) na ya watu binafsi

utasaidia kupunguza madhara yanayoweza kutokea. Aidha, matokeo ya tafiti kuhusu Mtazamo wa Soko na Maoni ya Watendaji Wakuu wa Taasisi (*The Market Perception and CEOs Surveys*) zilizofanyika Desemba 2025, yanaonesha kwamba uchumi utaendelea kukua, huku mfumuko wa bei ukiendelea kuwa tulivu.

SEHEMU YA SITA

6.0 SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA PILI YA MWAKA 2025/26

Tathmini ya mwelekeo wa mwenendo wa uchumi kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya Tano, unaonyesha mfumuko wa bei kuendelea kuwa mdogo, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, uchumi kukua kufikia asilimia 6.3 kwa Tanzania Bara na asilimia 7.2 kwa Zanzibar mwaka 2026. Ili kufanikisha malengo haya, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) iliamua Riba ya Benki Kuu (CBR) kubaki katika kiwango cha asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Machi 2026. Uamuzi kuhusu kiwango cha CBR ya robo ya mwaka inayoishia Juni 2026 itapangwa na MPC katika mkutano wake unaotarajiwa kufika wiki ya kwanza ya Aprili 2026. Kulingana na mwelekeo huo wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, kwa kutumia nyenzo zake za sera ya fedha. Utekelezaji wa sera ya fedha utalenga kuhakikisha riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa CBR.

Katika kuongeza ufanisi wa sera ya fedha, Benki itaendelea kufanya maboresho ili kuongeza ufanisi wa soko la fedha baina ya benki. Sambamba na hatua hizi, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha, ili kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha, ujumuifu wa huduma za kifedha pamoja na kuongeza matumizi ya malipo kidijitali. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya tafiti za kiuchumi, pamoja na kuboresha upatikanaji wa takwimu bora ambazo ni muhimu katika kufanya maamuzi ya sera ya fedha. Aidha, Benki Kuu itaongeza juhudi katika kuelimisha wadau kuhusu mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotegemea riba na kuendelea kuhakikisha wananchi wanafuata miongozo na kanuni zinazowataka kutumia shilingi katika kufanya miamala nchini.

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa kwa nguvu ya soko ili kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa mitaji hapa nchini, wakati CBR ikiendelea kuwa msingi katika upangaji wa viwango vya riba. Aidha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kufanya maboresho yanayolenga kuongeza uwazi katika upangaji wa riba, kuimarisha usimamizi wa benki na taasisi ndogo za fedha, kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha, na kuongeza elimu ya fedha pamoja na upatikanaji wa taarifa sahihi kwa umma ikiwemo kupitia utekelezaji wa mfumo wa kulinganisha riba na tozo za huduma za kifedha baina ya taasisi (price comparator system). Jitihada hizi zinalenga kuongeza ufanisi wa masoko ya fedha na hivyo kuchagiza ongezeko la mikopo.

Thamani ya ubadilishaji fedha za kigeni itaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko, na hivyo kuukinga uchumi dhidi ya athari zitokanazo na mitikisiko ya uchumi duniani. Benki itaendelea kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa kuzingatia Sera ya Ushiriki katika Soko la Fedha za Kigeni, ili kupunguza mabadiliko makubwa ya muda mfupi katika kiwango cha ubadilishaji wa fedha, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, na kufanikisha utekelezaji wa sera ya fedha. Vilevile, Benki itaendelea kuhakikisha kuwa washiriki wengine katika soko wanazingatia kanuni, miongozo na taratibu za soko la fedha za kigeni. Ili kulinda uthabiti wa thamani ya Shilingi, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha kuwa akiba ya fedha za kigeni inabakia ya kutosha na kufikia angalau miezi 4 ya uagizaji wa bidhaa na huduma katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2025/26. Hili litafanyika kupitia utekelezaji wa mikakati ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, ikiwemo ununuzi wa dhahabu kupitia mpango wa ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi.

VIAMBATISHO

Jedwali 1: Tanzania Bara: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

	2022				2023				2024				2025		
Shughuli za kiuchumi	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3
Kilimo	4.2	3.8	3.9	1.9	5.0	3.1	5.2	4.1	2.5	5.2	4.9	4.2	3.0	4.1	5.1
Uchimbaji madini na mawe	9.7	5.8	9.6	17.5	14.2	10.5	14.3	6.9	3.5	6.7	13.9	8.5	16.6	19.0	7.1
Viwanda	6.3	4.7	4.4	1.8	5.3	4.3	4.2	3.6	5.8	4.6	5.0	3.9	7.2	4.9	4.5
Umeme	9.4	9.6	9.7	2.3	3.6	6.2	3.3	2.7	7.6	11.0	15.0	23.9	19.0	14.0	13.6
Maji	11.9	9.5	0.1	2.2	5.1	3.3	1.8	0.1	3.1	3.5	3.7	5.9	4.2	3.7	4.4
Ujenzi	6.5	2.9	1.8	4.8	5.1	2.3	3.7	2.9	6.4	2.9	3.9	3.3	4.3	5.2	6.5
Biashara na matengenezo	7.2	6.7	1.9	0.6	2.7	4.1	4.3	5.8	5.3	3.7	4.8	5.4	3.5	5.5	6.4
Malazi na huduma ya chakula	1.5	13.0	13.2	8.5	12.3	7.2	7.4	6.7	7.2	5.5	5.8	5.7	2.3	3.9	6.7
Usafirishaji na uhifadhi mizigo	1.3	4.1	7.3	2.7	2.3	3.9	5.3	4.6	5.7	3.6	5.7	1.7	6.5	4.4	6.3
Habari na mawasiliano	5.9	6.4	10.8	6.8	3.5	6.2	11.3	9.7	14.6	12.9	14.5	15.1	7.8	11.1	12.3
Fedha na bima	9.6	9.7	8.7	8.9	12.3	14.0	16.8	15.5	14.9	14.1	14.5	12.1	15.4	14.8	14.2
Utawala na ulinzi	4.6	4.0	6.7	6.3	6.7	5.9	5.3	4.5	5.0	0.3	5.5	8.9	4.1	4.3	4.1
Shuguli za kitaaluma, sayansi na ufundi	5.0	5.5	6.8	5.9	5.3	4.7	4.1	8.0	4.5	4.8	4.2	5.6	5.1	4.2	4.9
Huduma zinazohusiana na utawala	6.0	5.2	3.6	3.7	5.5	5.8	5.6	2.9	5.2	5.2	6.1	8.3	3.7	3.1	3.8
Upangishaji majengo	4.5	4.4	4.4	4.4	4.1	4.2	4.2	4.6	4.2	4.3	4.3	4.3	4.3	4.3	4.4
Elimu	6.6	5.2	6.5	2.9	6.9	6.5	6.1	5.2	5.5	5.2	7.6	6.5	8.6	6.2	5.4
Afya	4.9	5.5	7.1	4.1	5.9	6.3	6.0	5.8	9.0	9.3	10.8	11.1	4.1	6.8	6.6
Sanaa na burudani	17.4	16.6	21.3	20.1	20.4	24.9	15.0	11.9	19.3	18.2	16.2	15.1	6.8	8.5	10.5
Huduma nyingine za kijamii	5.7	4.7	5.1	5.8	5.7	7.0	6.6	5.4	4.4	6.0	5.8	5.1	4.1	4.9	4.8
Shughuli zote za viwanda kwa bei za msingi	5.5	4.8	4.9	4.0	5.6	4.7	6.0	4.9	5.3	5.1	6.4	5.5	5.8	6.1	6.3
Kodi katika bidhaa	12.5	7.5	-0.5	-3.0	-1.5	6.2	2.5	7.9	3.7	5.9	2.2	4.4	-0.1	9.1	7.9
Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	6.0	4.9	4.5	3.4	5.1	4.8	5.7	5.1	5.2	5.1	6.1	5.4	5.4	6.3	6.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Jedwali 2: Zanzibar: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

	2022				2023				2024				2025		
Shughuli za kiuchumi	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3
Mazao	-9.5	-8.6	-3.2	20.5	10.4	6.1	3.7	1.6	7.1	13.1	2.5	3.7	17.7	1.5	5.8
Mifugo	-34.4	-9.6	-11.1	11.5	26.4	-5.2	-5.0	-28.3	-28.7	-20.0	-15.0	34.3	19.2	5.1	4.8
Misitu na uwindaji	3.8	3.7	2.0	4.3	9.7	7.5	-1.2	2.9	3.4	1.4	4.3	-1.4	-2.6	-1.6	1.2
Uvuvi	21.7	-5.8	47.5	93.9	5.5	-0.3	15.7	-17.3	7.2	29.2	22.8	-3.5	-5.7	5.1	6.4
Uchimbaji madini na mawe	19.1	15.0	1.9	18.7	37.4	41.4	0.6	-25.3	1.5	20.9	8.9	26.8	-14.2	4.3	5.4
Uzalishaji viwandani	9.2	3.1	0.5	14.3	5.9	4.5	2.2	7.1	5.1	4.2	5.8	-2.0	-9.7	1.7	2.7
Umeme	11.9	-9.6	20.1	8.0	0.2	19.6	12.1	30.3	7.9	9.4	0.6	10.2	9.0	8.1	7.9
Maji	5.0	6.5	1.1	6.6	4.8	6.8	3.0	0.4	4.6	-2.0	11.4	8.4	-0.3	1.7	3.2
Ujenzi	65.6	10.6	8.2	-14.1	22.7	7.2	23.9	-9.6	-5.0	14.4	10.4	-16.6	-3.0	-0.8	1.2
Biashara	3.0	15.7	1.8	17.5	33.5	2.0	-8.9	5.8	1.6	11.4	11.2	42.3	4.7	6.5	6.6
Malazi na huduma ya chakula	5.6	25.2	19.8	15.2	13.6	16.9	28.5	4.4	4.5	13.8	14.9	15.9	4.8	14.0	14.3
Usafirishaji na uhifadhi mizigo	-1.8	2.8	-3.8	11.6	11.9	21.4	3.3	3.7	1.8	4.2	-2.6	5.6	7.4	3.5	5.6
Habari na mawasiliano	-40.3	13.1	-11.1	0.0	32.1	-2.5	11.6	0.4	1.6	1.5	5.7	46.6	5.4	0.6	3.9
Fedha na bima	-0.2	11.5	4.7	12.7	92.8	30.4	0.1	69.0	7.4	0.3	6.0	-15.3	3.7	48.3	8.4
Upangishaji majengo	7.0	7.1	7.1	7.1	7.8	8.1	4.6	8.4	7.8	7.6	11.2	7.4	2.8	0.2	3.6
Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi	29.0	80.6	4.3	0.0	-27.8	41.3	14.2	0.0	4.9	19.5	2.0	-12.4	0.0	3.2	4.3
Huduma zinazohusiana na utawala	14.0	45.0	0.5	37.9	4.7	30.6	39.4	0.0	2.5	8.4	6.8	15.0	8.6	9.6	5.9
Usimamizi wa umma	4.5	-16.7	0.0	5.1	1.5	3.3	4.2	12.2	3.2	1.7	2.9	-10.3	4.3	3.2	2.4
Elimu	19.9	11.6	7.6	0.0	7.8	8.0	6.7	0.0	0.6	5.9	8.9	29.4	-3.2	7.5	3.2
Afya na huduma za jamii	-3.2	17.4	-0.4	5.2	27.2	-9.2	0.8	0.0	5.1	8.4	5.1	13.1	-8.7	9.7	2.7
Sanaa na burudani	5.5	63.8	37.8	0.0	17.2	33.8	-14.9	0.2	8.7	8.0	1.5	20.7	15.1	12.3	1.4
Huduma nyingine za kijamii	11.5	38.0	6.5	-20.5	-7.3	17.6	16.2	0.0	3.3	3.9	7.1	37.9	35.4	4.3	6.1
Huduma za ndani	3.2	3.2	3.2	0.0	3.2	2.4	1.6	0.1	3.2	3.2	3.2	9.8	3.2	3.2	3.2
Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM)	-18.9	6.0	-21.6	0.0	76.9	7.2	9.0	0.0	7.8	2.4	8.1	51.9	38.2	30.1	18.6
Shughuli zote za viwanda kwa bei za msingi	4.3	3.7	1.5	10.9	15.5	7.7	13.7	2.0	1.7	7.4	8.0	7.6	2.7	6.5	6.5
Kodi za bidhaa	13.1	38.0	-6.3	-31.2	6.6	-7.1	-7.5	6.0	2.8	6.1	2.7	1.1	43.3	9.6	12.5
Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	5.1	6.6	4.2	8.4	7.3	14.4	7.4	2.2	6.4	7.2	7.5	7.2	6.4	6.8	7.0

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar

Jedwali 3: Takwimu za Kifedha

Shilingi billioni

	Des-24	Jan-25	Feb-25	Mac-25	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Ago-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25
Rasilimali halisi za nje	13,558.2	12,688.5	14,706.2	15,442.1	14,658.6	14,028.1	15,509.5	15,726.1	15,766.0	15,896.7	15,715.4	16,298.6	15,283.5
Rasilimali halisi za ndani	35,346.8	37,146.0	35,942.2	36,699.8	38,679.1	39,313.4	39,973.8	40,565.0	41,689.9	41,957.4	44,073.3	44,560.0	46,240.8
Mikopo kwa sekta binafsi	36,097.4	36,576.1	36,982.7	37,999.3	38,755.8	39,792.0	40,549.0	40,972.2	41,530.9	41,999.9	42,386.9	43,385.5	44,584.6
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	48,905.0	49,834.5	50,648.4	52,141.9	53,337.7	53,341.5	55,483.3	56,291.1	57,455.9	57,854.0	59,788.6	60,858.6	61,524.3
Amana za fedha za kigeni (FCD)	11,765.3	12,419.3	12,818.2	13,605.9	13,846.3	13,543.4	13,769.3	13,653.2	13,696.3	13,337.2	13,882.1	14,056.5	13,381.1
Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)	*4,829.2*	*5,059.1*	*5,004.7*	*5,183.8*	*5,187.0*	*5,044.2*	*5,253.7*	*5,292.4*	*5,539.1*	*5,424.7*	*5,673.9*	*5,770.7*	*5,481.1*
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	37,139.7	37,415.2	37,830.2	38,536.0	39,491.4	39,798.1	41,714.0	42,637.9	43,759.6	44,516.8	45,906.5	46,802.2	48,143.2
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	22,905.5	23,073.0	23,118.8	23,541.7	24,013.1	24,214.9	25,653.9	26,231.6	27,402.4	27,916.4	29,058.1	29,184.1	30,199.0
Fedha zilizo kwenye mzunguko	7,351.6	6,997.7	6,954.5	7,190.0	7,024.1	7,438.9	7,874.8	8,122.1	8,036.4	7,730.8	8,410.1	8,545.0	8,492.3
Amana za hundi	15,553.9	16,075.4	16,164.2	16,351.7	16,989.0	16,776.0	17,779.1	18,109.4	19,366.0	20,185.6	20,648.0	20,639.0	21,706.7
Viashiria vingine													
Fedha Taslimu	12,024.5	11,670.3	12,078.7	11,793.1	11,878.9	11,800.7	12,451.7	13,423.8	13,537.9	13,717.6	15,068.7	15,135.7	14,508.3
Akiba za benki	3,351.5	3,516.5	4,038.2	3,623.1	3,738.7	3,364.8	3,533.1	4,131.4	4,402.3	4,721.7	5,462.8	5,436.9	4,642.9
Fedha zilizo nje ya Benki Kuu ya Tanzania	8,672.9	8,153.8	8,040.5	8,169.9	8,140.2	8,435.8	8,918.7	9,292.3	9,135.6	8,995.9	9,605.9	9,698.8	9,865.4
Wastani wa Fedha Taslimu	11,988.7	11,988.7	11,767.1	12,138.6	11,779.6	11,803.9	12,165.4	13,157.5	13,523.6	13,838.6	14,530.7	15,282.6	15,302.9
Kiwango cha ubadilishaji fedha (mwisho wa kipindi) (Shilingi ya Tanzania/Dola Milioni)	2,436.3	2,454.8	2,561.2	2,624.7	2,669.4	2,685.0	2,620.9	2,579.8	2,472.7	2,458.6	2,446.7	2,435.8	2,441.3
Viwango vya ukuaji wa kila mwaka (%)													
Fedha Taslimu	19.1	12.1	19.1	15.8	18.0	6.8	14.0	23.2	22.5	23.2	28.1	27.6	20.7
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	11.1	13.9	15.2	17.1	20.3	18.3	18.7	19.9	20.5	20.4	21.4	22.9	25.8
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	9.2	10.8	11.8	12.9	16.8	16.2	18.3	20.2	22.6	24.9	25.8	25.9	29.6
Mikopo kwa Sekta Binafsi	12.4	12.8	13.2	14.0	14.8	17.1	15.9	15.9	16.2	16.1	16.1	18.1	23.5

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali 4: Riba za Masoko ya Fedha na Mitaji

Asilimia

Aina ya riba	Des-24	Jan-25	Feb-25	Mac-25	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Ago-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25
Riba katika soko la fedha baina ya mabenki													
Siku 1 (Overnight)	7.07	7.69	7.87	7.91	7.90	7.95	7.93	6.62	6.15	6.29	6.45	6.08	6.00
Siku 2-7	7.38	7.74	8.02	8.02	7.98	7.96	7.96	7.43	6.52	6.43	6.29	6.19	6.30
Riba ya jumla	7.41	7.80	8.06	8.12	8.00	7.98	7.94	7.35	6.48	6.45	6.38	6.30	6.29
Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na Benki Kuu (Lombard rate)	8.00	8.00	8.00	8.00	8.00	8.00	8.00	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75
Riba ya mikataba ya mauziano ya dhamana za muda mfupi (Reverse REPO rate)	6.26	7.21	7.21	7.21	7.21	7.21	7.21	5.77	5.78	5.76	5.76	5.77	5.75
Riba ya dhamana za serikali													
Siku 182	8.30	8.20	8.20	8.20	8.47	8.24	8.24	8.24	7.46	6.56	6.41	5.92	5.91
Siku 364	12.95	12.63	11.99	10.11	8.92	8.92	8.92	8.13	6.79	5.99	6.00	6.45	6.24
Riba ya jumla	12.95	12.51	11.93	10.10	8.86	8.89	8.89	8.13	6.83	6.03	6.27	6.25	5.87
Riba za hati fungani za serikali													
Miaka miwili	11.64	11.64	12.55	12.55	12.08	12.08	12.08	12.17	12.17	12.17	10.05	10.05	10.05
Miaka mitano	12.41	12.41	12.41	13.14	13.14	12.94	12.94	13.18	13.18	12.48	12.48	10.54	10.54
Miaka saba	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71
Miaka kumi	13.26	14.08	14.08	14.08	14.26	14.26	14.26	13.74	13.74	13.74	12.45	12.45	12.45
Miaka kumi na tano	15.76	15.76	15.76	14.63	14.63	14.63	14.63	14.63	13.91	13.91	13.91	12.08	12.08
Miaka ishirini	15.71	15.71	15.28	15.28	15.11	15.11	14.50	14.50	14.50	13.55	13.55	13.55	12.02
Miaka ishirini na tano	15.93	15.84	15.84	15.84	15.84	15.29	14.80	14.80	14.42	13.19	13.19	13.19	13.19
Riba ya Benki Kuu	6.00	6.00	6.00	6.00	6.00	6.00	6.00	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali 5: Riba za Mabenki

Asilimia

Aina ya riba	Des-24	Jan-25	Feb-25	Mac-25	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Ago-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25
A: Shilingi ya Tanzania													
Riba za amana	2.84	2.97	2.98	2.86	2.89	2.52	2.90	2.90	2.90	2.92	2.93	2.88	3.02
Riba za jumla za amana za muda maalum	8.33	8.31	8.13	8.00	7.82	8.58	8.74	8.83	8.61	8.50	8.36	8.54	8.36
Miezi sita	9.30	9.86	9.40	9.68	9.36	9.82	10.28	10.28	10.44	10.12	10.06	10.01	9.96
Mwaka mmoja	9.62	10.08	9.48	8.14	9.27	9.72	9.79	9.88	9.99	9.84	9.21	10.02	9.58
Riba za amana za wateja wakubwa	10.39	11.80	11.40	10.35	10.52	10.64	11.21	10.72	10.99	11.05	11.22	11.67	11.66
Riba za mikopo za Jumla	15.71	15.73	15.14	15.50	15.16	15.18	15.23	15.16	15.07	15.18	15.19	15.27	15.24
Muda mfupi (Hadi mwaka 1)	15.74	15.70	15.77	15.83	16.15	15.96	15.69	15.51	15.64	15.52	15.50	15.53	15.46
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	16.79	16.89	16.06	16.56	16.33	16.35	16.49	16.41	16.45	16.26	16.42	16.42	16.42
Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3)	16.21	16.35	15.53	16.44	15.25	15.24	15.38	15.22	15.01	15.19	15.13	15.18	15.43
Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5)	15.24	15.25	14.09	14.32	13.88	14.19	14.35	14.39	14.02	14.26	14.24	14.43	14.29
Riba za mikopo za wateja wakubwa	12.83	12.80	13.42	12.94	12.88	12.99	12.68	12.56	12.72	12.84	12.40	12.61	12.38
B: Fedha za kigeni													
Riba za amana													
Amana za akiba	0.81	0.90	0.76	0.77	0.53	1.33	0.89	0.83	0.93	0.98	1.75	0.57	0.87
Riba za jumla za amana za muda maalum	4.20	4.22	3.66	2.98	2.94	3.65	3.60	3.75	4.11	3.94	4.17	4.03	3.67
Miezi sita	4.36	3.89	4.11	3.81	3.55	4.61	4.92	4.94	4.60	5.10	5.05	5.25	4.82
Mwaka mmoja	3.54	3.62	3.88	3.50	3.01	4.10	4.06	4.00	4.47	4.61	3.86	3.47	3.19
Riba za mikopo za Jumla	8.80	8.83	8.97	8.93	8.89	8.81	8.70	8.82	8.59	8.43	8.71	8.52	8.61
Muda mfupi (Hadi mwaka 1)	9.44	9.89	9.93	9.99	9.97	9.99	9.93	9.91	9.89	9.89	9.88	9.89	9.91
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	7.78	7.58	7.64	7.94	8.16	8.39	8.22	8.23	8.11	7.49	7.73	7.65	7.68
Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3)	9.19	8.81	8.57	8.28	8.23	8.49	6.88	7.03	7.16	7.25	7.43	7.49	8.31
Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5)	8.23	8.18	9.11	8.61	8.36	8.17	9.43	9.42	9.30	9.16	9.23	9.30	8.50

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Tafsiri ya Dhana Muhimu

Riba ya Benki Kuu

Ni kiwango cha riba kinachoamuliwa na Kamati ya Sera ya Fedha na kutumiwa na Benki Kuu kusimamia, kuashiria mwelekeo wa sera ya fedha.

Mfumuko wa Bei wa Msingi

Ni kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma, zisizohusisha nishati, vyakula visivyochakatwa na huduma za umeme na maji kwa kipindi maalum. Bidhaa za vyakula visivyochakatwa, nishati, huduma za umeme na maji hazijumishwi kwa kuwa bei zake hubadilikabadilika.

Uhimilivu wa Deni

Ni uwezo wa nchi kulipa madeni yake kwa wakati uliopo na baadaye bila kuhitaji msamaha wa deni au kuwa na malimbikizo ya madeni ambayo hayajalipwa (arrears). Kigezo muhimu cha kupima uhimilivu wa deni ni uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa (GDP).

Akiba ya Fedha za Kigeni

Akiba ya fedha za kigeni inajumuisha fedha na rasilimali zote za kifedha nje ya nchi ambazo zinasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Akiba hii hutumika kugharamia malipo ya nje, na pia kudhibiti kiwango cha nakisi ya urari wa malipo, kupitia ushiriki katika masoko ya fedha za kigeni. Akiba hii inajumuisha dhahabu-fedha inayomilikiwa na Benki Kuu ya Tanzania, haki maalum wanazopewa wanachama wa Shirika la fedha duniani (IMF) kutumia kiwango cha fedha za kigeni (Special Drawing Rights (SDRs), akiba ya fedha za kigeni katika Shirika la Fedha

la Kimataifa (IMF), pamoja na rasilimali za fedha za kigeni zilizopo Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kulipia bidhaa na huduma nje ya nchi.

Pato la Taifa (GDP)

Ni jumla ya thamani ya bidhaa na huduma zote zinazozalishwa katika uchumi ndani ya kipindi fulani. Bidhaa na huduma hizi huzalisha mapato halisi kwa uchumi ambayo hutumika ndani ya nchi au kwa ajili ya mauzo nje ya nchi. Pato la Taifa linaweza kupimwa kwa kutumia njia kuu tatu ambazo ni:

Uzalishaji – hupima thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa katika sekta zote za uchumi.

Matumizi – hujumuisha matumizi yote ya kaya, serikali, uwekezaji, na mauzo halisi ya nje.

Mapato – hupima mapato yaliyopatikana kutokana na uzalishaji, kama mishahara, faida, kodi na riba.

Mfumuko wa Bei

Kiwango ambacho wastani wa bei za bidhaa na huduma katika uchumi huongezeka kwa kipindi fulani. Kiwango hiki huwa kinawasilishwa kwa asilimia. Aidha, ongezeko la mfumuko wa bei huashiria kupungua kwa nguvu ya kununua au thamani ya fedha ya nchi husika.

Maoteo ya Mfumuko wa Bei

Ni makadirio ya matarajio ya kiwango cha mabadiliko ya fahirisi za bei kwa walaji (CPI) yanayofanywa na Benki Kuu, kulingana na tathmini ya hali ya uchumi wa ndani na mwenendo wa uchumi wa dunia. Makadirio haya hufanyika kwa kutumia uchambuzi kwa kutumia modeli za kiuchumi kwa kuzingatia utaalamu katika maswala ya kiuchumi. Kiashiria hiki huwasilishwa kama asilimia ya badiliko kwa mwaka.

Ujazi wa Fedha

Hujumuisha fedha zote zilizo kwenye mzunguko, nje ya mfumo wa kibenki na amana zote za wakazi wa hapa nchini zilizo kwenye mabenki. Kwa Tanzania ujazi wa fedha hutafsiriwa katika ngazi tatu ambazo ni ; Ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1), Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3).

- **M1** — Hujumuisha fedha zilizo kwenye mzunguko, nje ya mfumo wa kibenki pamoja na amana za hundi za wakazi zilizo katika mabenki.
- **M2** — Hii inajumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) pamoja na amana za akiba na za muda maalumu zilizo katika shilingi, zilizowekwa katika mabenki hapa nchini.
- **M3** — Ujazi wa fedha unaojumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na amana za fedha za kigeni zilizowekwa na wakazi kwenye benki ndani ya nchi.

Kiwango cha Soko cha Ubadilishanaji wa Sarafu (NEER)

Ni kipimo kinachoonesha thamani ya sarafu ya nchi ikilinganishwa na wastani wa sarafu za nchi mbalimbali ambazo ni washirika wake wa biashara. Kwa ujumla, NEER hutumika kutathmini kama sarafu ya nchi inaimarika au inashuka dhidi ya sarafu za nje, hivyo kutoa viashiria vya awali kuhusu ushindani wa bidhaa za nchi katika soko la dunia.

Mfumuko wa Bei Usio wa Vyakula

Ni ongezeko la bei za bidhaa na huduma zote isipokuwa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kilevi.

Mkopo Chechefu

Ni mkopo ambao umeshindwa kurejeshwa kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba kwa kipindi kinachozidi siku tisini (90). Pia, mkopo unaweza kuelezwa kama chechefu endapo umeonekana kuwa wa kiwango duni (*substandard*), wenye mashaka ya (*doubtful*), au wa hasara (*loss*) kulingana na vigezo vilivyowekwa katika Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Usimamizi wa Mali Hatarishi), 2014, au kanuni nyingine zinazoongoza taasisi za fedha au taasisi za huduma ndogo za fedha. Mara tu mkopo unapobainishwa kuwa mkopo chechefu, huondolewa kwenye utaratibu wa kutoza au kutambua riba (nonaccrual basis)

Deni la Serikali

Hujumuisha madai yote ambayo Serikali Kuu inapaswa kulipa au madai yote yaliyodhaminiwa na Serikali. Kwa upande wa Tanzania, deni la Serikali limegawanyika katika makundi mawili ambayo ni; deni la ndani ambalo huchukuliwa mahshusi kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti, na deni la nje (ambalo huchukuliwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo). Deni hili hujumuisha madai yote ambayo Serikali inapaswa kulipa kwa wakopeshaji wa nje pamoja na madeni mengine ya nje ya Idara na taasisi za serikali yaliyochukuliwa chini ya udhamini wa Serikali.

Kiwango Halisi cha Ubadilishanaji wa Sarafu (REER)

Ni kipimo kinachoonesha thamani ya sarafu ya nchi ikilinganishwa na wastani wa sarafu za nchi mbalimbali ambazo ni washirika wake wa biashara, baada ya kurekebishwa kwa kuondoa athari za mfumuko wa bei. Kipimo hiki cha huonesha ushindani halisi wa bei za bidhaa za nchi katika soko la dunia, kwa sababu huzingatia pia tofauti za mfumuko wa bei kati ya nchi.

Mikopo ya Muda Mfupi toka kwa Mabenki (Repo)

Ni utaratibu ambao Benki Kuu hukopa fedha kutoka kwa benki kwa kuuza dhamana, kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo pamoja na kiwango fulani cha riba baada ya muda maalumu kwa kuzinunua tena dhamana hizo kutoka kwa benki zilizokopesha. Utaratibu huu hutumika kupunguza ukwasi katika uchumi.

Mikopo ya Muda Mfupi kwa Mabenki (Reverse Repo)

Ni utaratibu ambao Benki Kuu hukopesha fedha kwa benki kupitia ununuzi wa dhamana kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo pamoja na kiwango fulani cha riba baada ya muda fulani, kwa kuziuza tena dhamana hizo kwa benki zilizokopeshwa. Utaratibu huu hutumika kuongeza ukwasi katika uchumi.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Jakaya Kikwete Road 40184,
Sanduku la Posta 2303, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 296 3182-7 or +255 26 22 223 2541
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz